**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA KWANZA - TAREHE 28 MACHI, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta ) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huu ni Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kwamba katika Mkutano wetu wa Pili wa Bunge pamoja na shughuli nyingine Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali mitatu. Miswaada hiyo napenda kuwafahamisha imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais tarehe 26 Machi, mwaka huu na sasa Miswaada hii ni sheria kamili za nchi yetu.

Wa kwanza ni *The National Leaders Funerals Act* namba moja wa mwaka 2006, *The Special Economic Zone Act* ya mwaka 2006 ambao utakuwa namba mbili na *The Export Processing Zones Amendments Act* ya mwaka 2006 ambao ni sheria namba tatu ya mwaka 2006.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI) :-**

Taarifa ya matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Elimu ya UKIMWI kwa Walemavu**

**MHE. MARGRET A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa janga la UKIMWI limeenea nchi nzima katika miji na vijiji na kwa kuwa makundi mbalimbali ya jamii; Serikali, Taasisi na Asasi mbalimbali zinaendelea kutoa elimu ya suala la UKIMWI kwa njia ya semina na makongamano na kwamba ushirikishi kwa watu wenye ulemavu katika elimu hiyo umekuwa haupo au ni mdogo sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kutoa elimu ya UKIMWI kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kwa vile watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali huhitaji mbinu tofauti tofauti kutumika ili kuwafikishia ujumbe au elimu ya aina yoyote ile kwamba sasa ni wakati muafaka kuwa na kitengo cha UKIMWI kwa watu wenye ulemavu ndani ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli UKIMWI ni janga ambalo liko kote hapa nchini na ndio maana kampeni dhidi ya maambukizi ya UKIMWI haina ubaguzi na inalenga kumfikia kila Mtanzania mahali alipo. Lakini kwa sababu ya ukubwa wa nchi yetu na rasilimali ambazo zinahitajika, kila mtu atafikiwa kwa awamu, mchakato unaotumika kutayarisha mpango wa maendeleo unaelezwa vizuri katika majukumu ya uendeshaji yaliyosambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa vikundi mbalimbali vya walemavu wanaombwa kufikisha mipango yao kwa Wakala wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI ambao wapo kila Mkoa au kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Mamlaka za Serikali za Mitaa au kwa Tume yenyewe ya Kudhibiti UKIMWI yaani *TACAIDS* ili ishughulikiwe mapema bila kuchelewa. Kwa njia hiyo tayari walemavu kadhaa wamesaidiwa katika vikundi vyao. Wengime wamesaidiwa na asasi zisizo za kiserikali kwa kushirikiana na Tume au asasi na wadau wengine kama sera inavyoelekeza.

(b) Mheshimiwa Spika, walemavu kupata na kuwa na elimu sahihi juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI ni haki yao. Hata hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kwa kuwa Tume huratibu tu

mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na siyo kutekeleza shughuli za kutokomeza UKIMWI, yenyewe haiwezi kuwa na vitengo vya vikundi maalum ikiwa pamoja na kundi la walemavu.

Tume kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeunda Kamati shirikishi za kudhibiti UKIMWI katika ngazi zote za mamlaka za Serikali za Mitaa. Imeteua pia Mawakala katika Mikoa yote. Asasi hizo ni pamoja na wadau wengine, zikiwemo asasi za walemavu, wanatakiwa kuibua matatizo na mipango endelevu ili ijumuishwe katika mipango ya Halmashauri husika kwa utekelezaji. Tume itaendelea kuratibu mipango hiyo kwa hali na mali na walemavu wanaombwa kuchangamkia mchakato huo ili uwanufaishe.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, UKIMWI ulianzia maeneo ya mijini na kwa sasa unaenea kwa kasi katika maeneo ya vijijini lakini mkakati mkubwa umekuwa ukiendelea katika maeneo ya ofisi, maeneo ya makazi ya mijini ambapo wakazi wa vijijini hawajawekewa mkakati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wa vijijini na wenyewe wakiwemo na hawa walemavu ambao pia tunao wanaweza kupewa elimu hii kwa uhakika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Ruth Msafiri, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa sasa kwa hakika Serikali imeeneza mtandao wa kudhibiti UKIMWI kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya hadi Vijijini. Hakuna sehemu hata moja ambayo sasa hivi suala la UKIMWI halijashughulikiwa. *(Makofi)*

Na. 2

**Posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanatambulika Kikatiba na wanafanyakazi kubwa sana lakini hawalipwi chochote na wengine wanatumia nyumba zao kuwapatia huduma wananchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwalipa posho Wenyeviti hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanafanya kazi kubwa ya kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Katika tangazo la Serikali Namba Tatu la tarehe 7 Januari, 1994 Halmashauri zote nchini zilielekezwa kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji si chini ya asilimia tatu ya makusanyo ya vyanzo vya mapato ambavyo Mwenyekiti wa mtaa amehamasisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kufuta kodi zenye kero na ambazo baadhi zilikuwa ni vyanzo vya mapato ya Halmashauri, bado kuna vyanzo vya mapato ambavyo Halmashauri zetu zinawajibika kuyakusanya. Aidha, kwa kutumia vema fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa, tuna uhakika kwamba Halmashauri zina uwezo wa kuwalipa posho Wenyeviti wa mitaa na vijiji kwa viwango wanavyostahili. Kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2000 hadi Juni, 2004, ililipa jumla ya shilingi milioni 5.6 kama posho kwa Wenyeviti wa Mitaa na vijiji. Aidha, Halmashauri hiyo hiyo katika Bajeti yake ya mwaka 2005/2006, imetenga jumla ya shilingi milioni 4 kwa ajili ya posho kwa Wenyeviti wa Mitaa. Aidha, zipo Halmashauri ambazo zinatekeleza agizo hili kwa hiyo tunaziomba Halmashauri nyingine ambazo hazijatekeleza agizo hili watekeleze hilo agizo mara moja.

Mheshimiwa Spika, wakati najibu sehemu ya swali namba 62 tarehe 15 Juni 2005, Wizara ilielezea na kusisitiza umuhimu wa kuwepo Ofisi za Watendaji wa mitaa na vijiji. Napenda kufafanua hapa kuwa majengo ya Ofisi hizo yanatakiwa yawe na sehemu kwa ajili ya viongozi yaani Wenyeviti wa mitaa na vijiji ili nao waweze kuhudumia wananchi wa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa kimsingi ni jukumu la wananchi wa ama mtaa au kijiji husika na Halmashauri za Wilaya na za miji nchi nzima kujenga ofisi hizo, kuimarisha uongozi na utendaji katika shughuli za maendeleo. Napenda kutoa wito na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwahamasisha wananchi na kuwashirikisha na viongozi wa Halmashauri juu ya ujenzi wa ofisi za kata na za vijiji.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa hali ya Serikali zetu za vijji inajulikana kwamba ni mbaya sana na kwamba mapato yake ni kidogo sana. Je Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika wa kuweka utaratibu wa kuwawekea posho Wenyeviti wa vijiji kama ilivyo kwa watendaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi tumeelekeza kwamba Halmashauri zote sasa hivi zitekeleze hilo agizo namba tatu ambalo limetolewa mwaka 1994. Agizo hilo linafahamika kinachongojewa ni utekelezaji tu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa sasa hivi inafahamika dhahiri kwamba vyanzo vyote vya mapato kwenye vijiji vinakusanywa na mawakala wa kutoza ushuru ambao wanapeleka pesa zote kwenye Halmashauri.

Sasa je, ni vipi vijiji vitaweza kulipa hizo posho za Wenyeviti wa Vijiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makusanyo yote yanakusanywa na mawakala na baada ya kukusanywa na mawakala asilimia fulani inarudi katika vijiji ile asilimia inayorudishwa ndiyo hiyo inalipwa kwa Wenyeviti wa vijiji. *(Makofi)*

Na. 3

**Viongozi Kuorodhesha Mali**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa maadili ya uongozi yanamlazimu kiongozi yeyote wa umma kuorodhesha mali zake zote pale anaposhika wadhifa wake.

Je, isingekuwa vema basi, kila kiongozi akatakiwa kuorodhesha tena mali zake, pale anapoacha wadhifa ili kujua kiasi gani cha mali na vipi amekusanya mali hii wakati wa uongozi wake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa viongozi wa umma kutaja mali zao umewekwa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliyotungwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1995 (Sheria Na.13 ya mwaka 1995). Viongozi wanaohusika na utaratibu huo ni wale wote walioorodheshwa katika kifungu cha 4(1) cha sheria hiyo pamoja na wale walioongezwa katika orodha kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na.209 la mwaka 2005. Sheria hii inawahusu viongozi wote waandamizi katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuweka utaratibu wa viongozi kutaja mali zao ni kuhakikisha kuwa viongozi hao hawatumii nafasi zao za uongozi kujilimbikizia mali isivyo halali na hawapati mali kwa njia za rushwa, ubadhilifu na matumizi mabaya ya madaraka yao. Aidha, sheria hii ina madhumuni ya kukuza na kuendeleza uadilifu wa viongozi na hivyo kudumisha utawala bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, kuwa ni vizuri kiongozi akatakiwa kuorodhesha mali zake anaposhika wadhifa na anapoacha wadhifa ili kujua ni kiasi cha mali aliyokusanya wakati wa uongozi wake. Aidha, kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma tayari kinamtaka kwamba kila kiongozi kufanya hivyo. Chini ya kifungu hicho kila kiongozi anatakiwa kutaja mali zake nyakati zifuatazo:-

(a) Katika kipindi cha siku thelathini baada ya kupewa wadhifa.

(b) Kila mwisho wa mwaka; na

(c) Mwisho wa kutumikia wadhifa wake.

Mheshimiwa Spika, kumtaka kiongozi kutaja mali zake mwisho wa kutumikia wadhifa kunatoa fursa kulinganisha alizokuwa nazo alipoanza kutumikia wadhifa aliokabidhiwa na zile alizonazo anapoacha wadhifa huu. Utaratibu huo unawezesha kufahamu kama mali alizonazo kiongozi huyo anapoacha wadhifa zinalingana na mshahara wake na mapato yake na hivyo kubaini kama alitumia cheo na madaraka yake kujipatia mali kihalali au isivyo halali.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ikiwa huyu kiongozi ni mmoja kati ya wale watakaoshika madaraka kwa miaka kumi na akionekana kwamba mali aliyojikusanyia ni kinyume cha mshahara wake na marupurupu yake. Je, huoni kama kuna haja ya kiongozi huyo mstaafu kupelekwa mahakamani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kila mwaka viongozi waliotajwa kutoa taarifa za mali zao na mtiririko huo hufuatwa kwa muda wa miaka mitano hadi miaka kumi. Hivyo katika miaka kumi kama kuna ushahidi wa kutosheleza kwamba mali iliyopatikana kwa njia isiyo halali raia mwema yeyote anaweza kufungua kesi mahakamani.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kujua ni viongozi wangapi kama wapo ambao wamewahi kukiuka maadili haya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, toka sheria hii ianze kutumika kwanza hakuna mtu yeyote au mwandishi yeyote wa habari aliyewahi kuomba kuchunguza jalada la kiongozi yeyote hivyo hakuna aliyewahi kushitakiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 4

**Takrima kama Rushwa**

**MHE. KABWE Z. ZITTO ( k.n.y. MHE. PHARES K. KABUYE)** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya miiko ya Taifa letu ni mtu kutoa/kupokea rushwa; na kwa kuwa katika kipindi cha uchaguzi watu wengi huhonga wapiga kura kwa kisingizio cha takrima na kusababisha wasio na cha kutoa wasichaguliwe hata kama walistahili;

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kitendo cha mtu kutoa takrima ili achaguliwe ni kitendo cha rushwa na takrima wakati wa kampeni za uchaguzi inastahili kutungiwa sheria ya kuipiga marufuku kabla nchi yetu haijatekwa nyara na kuongozwa na wenye nacho tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kabuye, Mbunge wa Biharamulo kama ifuatavyo:-

Kwa sasa Sheria inayotumika kuendesha shughuli za uchaguzi chini ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa ni Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 (Sheria Na. 1 ya mwaka 1985) kama ilivyorekebishwa mara kwa mara. Sheria hii iliporekebishwa mwaka 2000; kifungu cha 98 kilichoweka masharti ya vitendo vinavyokatazwa ili kushawishi mtu kupiga kura au kutopiga kura kilifanyiwa marekebisho ili kutoa ufafanuzi zaidi katika kifungu cha (2) na (3) ili ieleweke wazi kuwa:

"Kitu chochote kitakachofanywa kwa nia njema ikiwa ni kitendo cha kawaida au ukarimu wa kimila/asili hakitachukuliwa kama kosa la rushwa. Pia, gharama za matumizi ya kawaida yaliyotumika kwa nia njema katika kampeni za uchaguzi au shughuli za kawaida za uchaguzi hazitachukuliwa kama kosa la rushwa."

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa malalamiko kuhusu matumizi mabaya ya ruhusa ya ukarimu wa kimila. Yapo madai kwamba wapo wanaotumia fursa hiyo kununua jambo ambalo ni kinyume. Kwa kutambua kuwepo kwa

hofu hiyo, Serikali inaona suala hilo litazamwe upya ili kama upo mwanya wa kutumika vibaya, uzibwe.

Mheshimiwa Spika, ni makusudio ya Serikali kuanzisha mjadala nchini kuzungumzia suala hili ili tuelewane kuhusu kasoro zilizopo na hatua za kuchukua. Ni matumaini ya Serikali pia kwamba tutaelewana utaratibu halali na ulio wazi wa Chama au mgombea kutafuta au kupata fedha za uchaguzi na kutumia fedha hizo katika uchaguzi. Makubaliano au maamuzi yatakayofikiwa yatakuwa sehemu ya Sheria ya Uchaguzi. Maandalizi ya zoezi hilo yanaendelea.

Ni matumaini yangu kuwa viongozi, wanachama wa Vyama vyote vya Siasa na raia kwa ujumla, watatoa michango yao ya mawazo pindi mjadala huo wa kitaifa utakapozinduliwa rasmi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:- Kwa kuwa tatizo la takrima kwenye uchaguzi limeanza kujadiliwa toka mwaka 2000 baada ya Sheria ya Takrima kuruhusiwa na kwa kuwa tayari vitendo vya rushwa vimezaa viongozi ambao wameingia madarakani kwa rushwa na kwa kuwa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake hapa Bungeni alizungumzia suala la kupinga viongozi kununua uongozi, je, Serikali haioni sasa ni wakati rasmi wa kuleta Sheria ya kupinga takrima badala ya kuendeleza mjadala ambao tayari umekwishajadiliwa toka mwaka 2000? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Kwanza hakuna uthibitisho au ushahidi tulionao kwamba kuna viongozi walionunua ushindi. Katika swali la msingi wakati wowote kuanzia sasa tunataka kuibua mjadala wa Kitaifa kuhusu namna bora zaidi na namna adilifu zaidi ya namna ya kuendesha chaguzi zetu ndani ya vyama na Serikali kwa ujumla ili wananchi wawe na hakika kwamba viongozi wao wametokana kihalali.

Mheshimiwa Spika, namkaribisha Mheshimiwa Kabwe Zitto, wanachama wa chama chake, wapiga kura wake na wananchi kwa ujumla pindi mjadala huo utakapozinduliwa watupe mchango wao wa mawazo. *(Makofi)*

Na. 5

**Utupaji wa Watoto Wachanga**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE** aliuliza:-

Kwa kuwa binadamu anayohaki ya Kikatiba na ya msingi ya kuishi; na kwa kuwa hivi sasa umezuka mtindo wa kuwatupa na kuwaua watoto wachanga na kuwanyima haki yao ya msingi ya kuishi:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge na umma wa Watanzania kwa ujumla sababu zinazowafanya wazazi husika kuwatupa au kuwaua watoto wao?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza kwamba hadi kufikia mwezi Desemba, 2005 ni watoto wangapi wametupwa/wameua kutokana na ukatili huo?

(c) Je, Serikali inatoa adhabu gani kwa wanaofanya vitendo hivyo ili kukomesha kabisa vitendo hivyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a), (b), na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya wazazi ambao huwatupa au kuwaua watoto wao wachanga mara wanapozaliwa au baada ya kuzaliwa na kuwanyima haki yao ya msingi ya kuishi.

Tatizo hili hutokana na sababu nyingi zikiwemo za wazazi kupata ujauzito katika umri mdogo na mara nyingi kukataliwa na baba wa mtoto ama kuogopa kugombezwa na wazazi au kufukuzwa baada ya kujlikana kuwa ni wajawazito.

Aidha, matatizo mengine ni kama matatizo ya familia, ujauzito usiotarajiwa, umasikini uliokithiri, uzazi usio kuwa na mpangilio, kuvunjika kwa ndoa na kifafa cha mimba na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu za watoto waliotupwa au kuuawa na wazazi au walezi wao ni vigumu kupatikana kiusahihi kwani mengi ya matukio hayo hufanywa kwa kificho au usiri mkubwa. Takwimu zilizopo chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii ni kwamba katika mwaka 2005, idadi ya watoto 350 walitupwa sehemu mbalimbali nchini na asilimia 45 ya watoto hao walitupwa katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, adhabu zinazotolewa kwa wanaofanya vitendo hivi zinatofautiana kulingana na uzito na mazingira ya kosa lenyewe. Kwa mfano, wanaotupa watoto kutokana na kuchanganyikiwa au kifafa cha mimba huwa chini ya uangalizi wa afisa ustawi wa jamii hadi mwaka mmoja kulingana na mazingira ya tukio lenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama mazingira ya kosa lenyewe inadhihirika kufanywa makusudi na katika shauri mkosaji akaonekana na hatia hufungwa kifungo cha kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitatu kwa mujibu wa sheria.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa ya kutoa elimu kwa Watanzania wote itakayosaidia kuzuia kuzuiwa kubeba mimba zisizohitajika?

(b) Hadi wakati huo elimu itakaposambaa na kutekelezwa na wote, je, Serikali haioni iko haja ya kujenga vituo vya kukusanyia watoto hawa wakiwa hai ili waendeleze uhai wao? Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, kama ifuatavyo:-

Kuhusu elimu ya uzazi inatolewa sasa katika maeneo mengi, inatolewa na vyombo vya habari na pia inatolewa katika shule za sekondari. Hata hivyo kwa wale ambao hawapo katika shule za sekondari, elimu hii wanaipata kwa njia ya *radio* na pia katika vituo mbalimbali vya afya ambavyo vinatoa elimu hiyo. *(Makofi)*

Swali la pili, ni kweli watoto hawa wanapopatikana hukusanywa na kupelekwa katika vituo mbalimbali hapa nchini vituo ambavyo vipo katika kila Mkoa ambavyo vingi viko chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mtoto hupatikana kwa kushirikiana na baba na mama na kwa kuwa baba wengi huwatelekeza mama na watoto pale wanapoona wamejifungua hawa watoto kwa sababu tofauti kama alizozieleza Mheshimiwa Waziri na ndiyo maana wanawake wengi huwatupa hawa watoto kutokana mazila wanayopata kutokana na hawa baba.

Je, likithibitika hilo baba wa mtoto na yeye anapewa adhabu gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, baba ambaye atampa mimba mwanamke na kukimbia kama akijulikana atachukuliwa hatua za kisheria. Lakini mara nyingi ni vigumu kujua ni nani ambaye amempa hiyo mimba. Lakini kwa sasa kwa kuwa Serikali imeweza kupata mashine ambayo inaweza kutambua mtoto ni wa nani, hii itatusaidia kama wao wakienda mbele ya sheria na kuwashitaki. *(Makofi)*

Na. 6

**Watoto Yatima na Wasiojiweza**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna watoto wengi ambao ni yatima na wasiojiweza nchini Tanzania; na kwa kuwa Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwalipia gharama za masomo watoto hao wote, lakini kinyume chake Serikali za Vijiji zimekuwa zikichuja watoto hao yatima na wasiojiweza kufuatana na idadi inayotakiwa na Wilaya kwa kigezo kuwa pesa ni kidogo:-

(a) Je, hao watoto wanaobakia bila kuchaguliwa Serikali haioni kuwa inawanyima haki yao ya msingi?

(b) Je, ni lini watoto hao waliobakia watapatiwa msaada wa kusomeshwa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, naomba nitoe maelezo mafupi.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto, kama inavyoelekezwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto na kwa kutambua hilo, Serikali yetu inayoongozwa na sera nzuri za Chama cha Mapinduzi, imehakikisha kuwa elimu ya msingi inapatikana bure kwa watoto wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nimjibu Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, maswali yake kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ina utaratibu wa kuwalipia gharama za masomo baadhi ya watoto wasiokuwa na uwezo, wakiwemo watoto yatima waliochaguliwa kwenda shule za sekondari za Serikali. Aidha, Serikali imeweka vigezo vya kuwalipia gharama za masomo watoto hao kwa nia njema kabisa ili kuhakikisha kuwa watoto wanaopata msaada huo ni wale tu wanaostahili, kwa mfano, wapo watoto ambao ni yatima lakini wana ndugu wa karibu wenye uwezo wa kuwasomesha. Pia wapo watoto yatima ambao wamefiwa na wazazi wote au mmoja lakini ndugu waliopo hawana uwezo wa kukidhi mahitaji ya watoto hao.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wa kundi hili ndio wanaopewa kipaumbele cha kusaidiwa na Serikali. Hata hivyo tatizo hili la watoto yatima sio la Serikali peke yake, bali ni la jamii nzima hivyo jitihada za pamoja zinahitajika ili kuhakikisha kuwa watoto hawa wanapata elimu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama sehemu ya jamii tusaidie kubainisha yatima wenye matatizo zaidi, kwani nafasi hizo hutumiwa vibaya sehemu nyingine. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kundi la watoto wanaoshindwa kuendelea na masomo ya sekondari ni kubwa wakiwemo na watoto yatima. Jitihada za Serikali kubeba mzigo huu zinaendelea.

Hata hivyo, Idara ya Ustawi wa Jamii katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetenga fungu maalum kwa ajili ya kuwalipia watoto yatima ambao wanakidhi vigezo vilivyowekwa. Aidha, Idara ya Ustawi wa Jamii, huwasiliana na wafadhili pamoja na asasi mbalimbali katika kuongeza uwezo wa fungu hilo.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Kata na Wilaya vilishachagua awamu ya kwanza, *(first selection)* na kwa kuwa watoto wanaochaguliwa *second selection* huwa hawapati nafasi hiyo; Je, Serikali ina mpango gani juu ya hao watoto?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto ambao wanasubiri *second selection* jitihada zinafanywa na agizo limetolewa na Waziri Mkuu kwamba kila Kata ijitahidi kujenga Shule zaidi ili watoto hawa waweze kuingia katika *second selection. (Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, tatizo ambalo sisi tunaliona kule Vijijini ni kwamba Bajeti inayotolewa kwa ajili ya kuwasaidia hawa yatima ni ndogo na haiwezekani kutegemea kuwapa jamii ambayo wao wana watoto wao vile vile wabebe mzigo huu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuahidi kwamba wataiangalia tena Bajeti ili watoto wote wanaostahili kupata msaada wa Serikali wapate? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tatizo la malezi ya watoto yatima ni letu sote jamii na kwa kuwa vituo havina uwezo wa kutunza watoto wote, ni wajibu wetu jamii kuhakikisha tunawasaidia watoto hawa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango kama tunavyochangia harusi ndugu na jamaa. *(Makofi)*

Natoa rai kwamba sisi kama Wabunge, tuna nafasi kubwa ya kuweza kuwasaidia hawa yatima kwa kuwatambua kwanza na kutafuta asasi zisizo za Serikali ili watusaidie katika maeneo yetu. Nitatoa mfano mmoja, jana tumeona katika radio Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Kilosa alitoa magunia ya mahindi na aliwafungulia akaunti

ya shilingi 300,000/= watoto yatima. Kwa hiyo, natoa rai kwamba Wabunge tuwe karibu sana na Vituo na tuwe karibu sana na kujua watoto yatima maslahi yanaendaje. *(Makofi)*

**Na. 7**

**Ujenzi wa Daraja katika Mto Songwe**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Lusungo kilichopo katika Kata ya Ruanda, Tarafa ya Iyula kinatenganishwa na Mto Songwe na kwa kuwa, wananchi wa Kijiji hicho hulazimika kupitia Mbeya Vijijini wanapotaka kwenda Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu hakuna Daraja la kukiunganisha Kijiji hicho na Kijiji cha jirani cha Songwe - Mbozi; na kwa kuwa, mto huo ni mpana sana na ni vigumu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kujenga daraja la kuunganisha Vijiji hivyo viwili:-

Je, Serikali Kuu ina mpango gani wa kujenga daraja la kuunganisha Kijiji hicho cha Lusungo na sehemu nyingine za Wilaya ya Mbozi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Songwe ni mpaka kati ya Wilaya ya Mbeya Vijijini na Mbozi katika Mkoa wa Mbeya. Aidha, mto huo unatenganisha Kijiji cha Lusungo kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Kijiji jirani cha Songwe.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Kijiji cha Lisungo, hulazimika kupita Wilaya ya Mbeya Vijijini ili kwenda Makao Makuu ya Wilaya yao ya Mbozi kwa sababu ya kukosekana kwa daraja katika Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa fedha, Wizara yangu haiwezi kusaidia ujenzi wa daraja hilo kwa sasa. Namshauri Mheshimiwa Godfrey Zambi awasiliane na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ili iweke mkakati wa kujenga daraja na barabara ya kuunganisha Vijiji hivyo. Aidha, Wizara yangu itakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalam endapo itaombwa kufanya hivyo.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi hawa wa Lusungo wanaijua Serikali moja, hawajui mgawanyo huu wa Wilaya ya Mbozi, Halmashauri na Serikali Kuu na vile vile wananchi hawa hawajui mgawanyo wa fedha ya *Road toll* kwamba ni nani anapata zaidi; Je, Serikali itakuwa tayari kuwasaidia watu hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wananchi hawaelewi mgawanyiko huo, ni jukumu letu sisi kama Wabunge na Halmashauri ya Wilaya husika kuwapa elimu inayohusika. Lakini kubwa ni jukumu la Halmashauri hiyo kuona kwamba tatizo hilo kama ni kubwa kiasi hicho, basi waweke kipaumbele ili daraja hilo na barabara hiyo iwekwe kwenye Bajeti ya Halmashauri itumwe *TAMISEMI* na hatimaye iweze kujengwa ili wananchi wasipate matatizo zaidi. *(Makofi)*

**Na. 8**

**Matumizi ya Mti wa Mbuyu**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa majibu yalitolewa na Waziri wa Afya Bungeni katika Bunge mwaka 2000-2005 kuhusu matumizi ya mti wa Mbuyu yalisababisha wananchi wengi kuhamasika kutumia mti huo kwa tiba ya magonjwa mbalimbali na kwa kuwa, wananchi wengi hutumia tiba hiyo bila vipimo vyovyote:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa matumizi hayo bila vipimo yanaweza kusababisha athari kwa watumiaji?

(b) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa kugundua maradhi yanayotibiwa zaidi kwa mti huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud,Mbunge wa Koani, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mti wa mbuyu kitaalam unaitwa *adansonia digitata* au *adansonia sphaerocarpa.* Wananchi wa hapa nchini na nchi nyingi za Kiafrika hususan Afrika Magharibi wamekuwa wakitumia matunda yake (ubuyu) na majani ya mti wa mbuyu kama dawa ya maradhi mbalimbali. Matokeo ya tafiti zilizofanyika zinaonesha kwamba mti huu una vitamini A na C kwa wingi pamoja na viini vingine ambavyo bado vinafanyiwa utafiti kuvitambua. Inasadikiwa kuwa vitamini hizo na viini vinafanya kazi kama virutubisho kwa kusaidia kuongeza uwezo wa mtu kuhimili maradhi na kumfanya mtumiaji asiugue kwa urahisi na yule anayetibiwa apone haraka. Hadi sasa hakuna ripoti yoyote ya madhara kwa binadamu yanayoweza kusababishwa na utumiaji wa ubuyu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli matumizi ya dawa yoyote bila ushauri wa kidaktari yanaweza kuleta athari kwa mtumiaji, lakini kwa upande wa ubuyu matumizi yake hayajawahi

kuunganishwa na athari kwa binadamu. Hata hivyo, iwapo madhara yatajitokeza Wizara yangu itayafuatilia ili ushauri muafaka uweze kutolewa.

(b) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, haijafanya utafiti wowote kuhusu mti wa mbuyu. Lakini katika kujiandaa kwa utafiti huo Taasisi ya Madawa Asilia imeamua kuanza kupanda mibuyu ambayo itakatwa ili kuzuia kurefuka na kubakia kimo cha kuweza kuchuma majani kwa ajili ya utafiti. *(Makofi)*

Na. 9

**Upimaji wa Viwanja vilivyojengwa bila Kupimwa**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu aliahidi kuwa wananchi wote waliojenga kwenye maeneo yasiyopimwa hasa mijini watapimiwa maeneo ya nyumba zao na kupewa hatimiliki ili kuwawezesha kuweka dhamana ya nyumba zao wanapotaka mikopo kwenye benki zinazokopesha:-

(a) Je, zoezi hilo limefikia wapi na nini kinachoendelea sasa?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani kwa wananchi ambao hawatakuwa na hatimiliki za nyumba zao kwenye maeneo husika?

(c) Je, kama mtu anataka kuifanyia ukarabati nyumba yake kwenye maeneo hayo au kujenga nyuma npya katika eneo lake akiwa tayari anayo hati miliki, atatakiwa kufuata hatua zipi kabla ya kuanza kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuyatambua maeneo yaliyojengwa bila kupimwa na kuwapa wananchi wanaomiliki leseni za makazi *(Residential License)*. Kazi ya kuwatambua wakazi waliojenga kwenye maeneo yasiyopimwa imefanyika katika Jiji la Dar es Salaam ambapo jumla ya miliki 210,000 zilitambuliwa na leseni za makazi 20,000 zimetolewa kwa wamiliki wa maeneo hayo. Pia kazi kama hiyo imefanyika Jijini Mwanza, Manispaa ya Dodoma na itaendelea mijini katika mikoa mingine nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa hatimiliki kwa wananchi wanaostahili kwenye maeneo yasiyopimwa mijini baada ya kukamilika kazi ya kuyatambua maeneo hayo na urasimishaji *(regularization)*. Hata hivyo, mpango wa kutoa hati za kumiliki ardhi haukuwa kwa watu wote waliojenga kwenye maeneo yasiyopimwa kama

ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge. Baadhi ya nyumba zitaondolewa ili kupisha ujenzi wa Miundombinu kama barabara na mifumo ya majitaka na wananchi wakaoondolewa watapatiwa viwanja kwenye maeneo mengine. Pia wananchi waliojenga kwenye maeneo hatari kama vile mabondeni hawatanufaika na mpango huu.

(c) Mheshimiwa Spika, mabadiliko yoyote yaliyokusudiwa kufanywa kwenye nyumba yenye hatimiliki na iliyotolewa kibali cha ujenzi, ni lazima yafuate taratibu zilizowekwa na Halmashauri za Miji na Wilaya.

(d) Halmashauri za Miji na Wilaya ndizo zenye mamlaka ya kutoa vibali vya ujenzi au ruhusa ya kuifanyia ukarabati nyumba katika eneo husika. Mara mchoro wa ujenzi au ukarabati unapowasilishwa kwao, wataangalia mpango wa uendelezaji wa eneo husika na kuhakikisha kuwa ujenzi unaokusudiwa unazingatia matumizi ya ardhi yaliyokubalika. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imetamka kwamba Serikali iliyoko madarakani itapima nyumba za wananchi vijijini pamoja na mashamba yao na kuzipa hatimiliki na kuzitambua na Mabenki yazitambue ili wananchi waweze kupata mikopo. Je, utaratibu huo utaanza lini naomba useme na wananchi wangu wa Nyang'hwale wasikie? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 tumesema kwamba tutapima nyumba na ndiyo nimejibu katika swali la msingi na tayari Mikoa mitatu wamekwishaanza kupima nyumba na kutoa leseni. Nitakupa tarakimu kidogo, mpaka sasa tumepima nyumba 210,000 na tayari wamekwishaanza kutumia hizo leseni kwa kupata mikopo kutoka Benki za *CRDB, SACCOS* mbalimbali na bado Mabenki mengine tunawasiliana nao kukubali leseni ambazo zinatolewa. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wamesema kwamba utaratibu huu umeendelea kufanyika hasa inavyoonekana ni katika miji mikubwa na tayari kwa takwimu ambazo zimesemwa na Naibu Waziri, zinaonyesha kwamba watu wameanza kupata hatimiliki kwa ajili ya kuchukua mikopo katika Benki na watu wanaoishi katika miji mikubwa na kwa kuwa Wilaya ya Bukombe ni moja ya Wilaya ambayo haijapata kabisa hatimiliki katika majengo yake pamoja na wananchi kujitahidi kujenga nyumba nzuri katika eneo hilo.

Je, Serikali inaweza ikawahakikishia wananchi ni lini watapimiwa na kupewa hatimiliki katika maeneo yao ili na wao waweze kupata maendeleo kwa kupata mikopo kwenye Mabenki hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mikakati ya kupima nyumba zote nchi nzima na siyo miji mikubwa tu. Lakini kama nilivyosema hapo awali ni kufuatana na uwezo wa kifedha.Tutahakikisha tumehamasisha Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ili

waweze nao kutafuta fedha na kuanza kupima kwa sababu hii ni katika mradi wa MKURABITA ambao tunajaribu kutekeleza kwa kipindi cha miaka mitano. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Kwa kuwa zoezi hili limeanzia katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mwanza na kwa kuwa nimekuwa nikipokea maombi mengi kwa wakazi wa Jimbo la Kigamboni, ili wapate uwezo wa kwenda kukopa; je, zoezi hili limesita kwa kiwango gani kwa Dar es Salaam mpaka sasa limeshindwa kuendelea kufika katika Jimbo la Kigamboni na Serikali ina mpango gani kuendelea hadi kufika katika jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam umefaidika sana na zoezi hili, tumeanza Wilaya ya Kinondoni, Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Temeke. Katika Wilaya hizi tatu Kinondoni ni nyumba 62,000, Ilala 52,000 na Temeke nyuma 100,002.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea kwamba tumeanza zoezi katika eneo lenye msongamano wa nyumba kwa mfano Mbagala, Mtoni katika Wilaya ya Temeke na tutaendelea na Kigamboni ambako kwa kusema kweli sasa hivi mashamba ndiyo mengi katika jimbo lako. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi linaendelea vizuri sana katika Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Na. 10

**Maeneo Yasiyotumika kwa Muda Mrefu**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (k.n.y. MHE. MBARUK K. MWANDORO)** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo maeneo mengi ya ardhi katika Wilaya ya Mkinga ambayo yamebakia bila kutumiwa kwa sababu ya kukodishwa kwa muda mrefu kwa wakulima, wakubwa mashamba ya utafiti, maeneo ya Majeshi, na kadhalika na kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ni kujenga uchumi wa kisasa unaojitegemea na kuruhusu wananchi kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao.

(a) Je, isingekuwa busara kwa Serikali kukagua maeneo mbalimbali nchini ambayo hayajatumika kwa muda mrefu bila sababu ya kuridhisha na kuyagawa upya kwa wananchi walio tayari kuyatumia kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla?

(b) Je, upo uwezekano gani wa Serikali kuwashurutisha wamiliki wa ardhi hiyo wazitumie ipasavyo, kama sheria hairuhusu kugawa hayo maeneo?

(c) Je, Serikali inaweza kutoa taarifa Bungeni juu ya maeneo halisi yaliyobainika kutotumika kwa muda mrefu na hatua ambazo zimechukuliwa au zinazotarajiwa kuchukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera, Sheria na Kanuni za Ardhi, Serikali imekuwa ikitekeleza jukumu la kukagua maeneo ya mashamba na viwanja nchini na kuhimiza uendelezaji kwa mujibu wa masharti ya umilikaji. Iwapo itabainika mmiliki amevunja masharti ya umilikiaji, Halmashauri za Miji na Wilaya kwa kushirikiana na Mkoa huwasilisha mapendekezo kwa Kamishna wa Ardhi, ili Waziri mwenye dhamana na ardhi amshauri Mheshimiwa Rais akubali kufuta hatimiliki zilizo hai. Mheshimiwa Rais akisha kubali, hatimiliki zilizopendekezwa zitafutwa na ardhi hiyo itagawiwa kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria za Ardhi na Kanuni zake. Kazi hiyo inafanyika nchini kote ili wananchi waweze kuelewa na kutekeleza masharti ya umilikaji yaliyoainishwa. Aidha, Serikali imekuwa ikiwashauri wamiliki wa ardhi kuyatumia maeneo yao kikamilifu na wanaposhindwa kuendeleza eneo lolote au sehemu ya ardhi hiyo hatimiliki ya shamba lote hurejeshwa Wizarani na kumega sehemu au kugawa shamba lote kwa watumiaji wengine kwa mujibu wa Sheria kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 sehemu ya pili *(Sub-Part 2: Conditions on Right of Occupancy)* na sehemu ya tatu *(Sub- Part 3 Dispositions of Right of Occupancy)*. Pia kulingana na matakwa ya sheria hizo, Halmashauri za Miji na Wilaya zinawajibika kulipa fidia ya ardhi na mazao kwa wamiliki wa mashamba yanayopendekezwa kufutiwa hatimiliki.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaanza kuhuisha takwimu za viwanja na mashamba nchini kote. Hatua za awali zitakamilika mwezi Mei, 2006. Maana kazi ya kubaini na kupitia ushauri wa kufuta hati miliki kama itakavyopendekezwa na Halmashauri za Miji na Wilaya kwa kushirikiana na Mkoa, taarifa zitatolewa kwa wadau husika wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Hadi Machi, 2006 Wilaya ya Mkinga kwa kushirikiana na Mkoa walikuwa hawajawasilisha mapendekezo ya kufuta hati miliki zilizo hai za mashamba yaliyopo kwenye eneo yao. Lakini kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, katika Wilaya ya Muheza ambapo iko na Wilaya mpya ya Mkinga kuna mashamba yafuatayo ambayo hayajatumika kwa muda mrefu:-

(i) Sehemu ya Shamba la JKT Maramba;
(ii) Shamba la Kilulu;
(iii) Shamba la *Moa Estate;* na
(iv) Shamba la Mbegu la Maramba.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wilaya na Mkoa tutafanya uchunguzi wa kuona kilichofanya yasiendelezwe ili hatimaye sehemu ya mashamba hayo ipendekezwe kumegwa au kufuta miliki zote. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika kubinafsisha mashamba yaliyokuwa ya Serikali katika zoezi la ubinafsishaji imejitokeza waziwazi kwamba kuna wawekezaji ambao wamepewa mashamba haya lakini nia yao kwa kweli haikuwa kuyaendeleza ila ni kuingiza ukiritimba wa ardhi. Je, Serikali itahakikisha kwamba inachukua hatua kuhakikisha kwamba waliopewa mashamba hayo hawayatumii tu kama limbikizo la ardhi bali ni kuyaendeleza? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inazingatia kwa karibu sana watu waliopewa mashamba wakati wa ubinafsishaji na hawakuyatumia. Mfano katika Wilaya ya Muheza kuna Shamba la Kilulu ambalo mwanzo alipewa mwekezaji anaitwa Jiwer ambaye ni mwingereza na sasa anaishi Kenya akanyang'anywa akapewa Chavda naye akanyang'anywa vile vile wakapewa *Mbegu Technologies* na eneo lingine sasa hivi linashughulikiwa liweze kuwa Wilaya mpya ya Mkinga pamoja na wananchi waweze kupewa sehemu ya shamba hilo. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza kwamba sheria iliyokuwa inatumika kabla ya mwaka 1972 wakati wa kuwakusanya watu katika Vijiji ilikuwa inaruhusu wananchi kumiliki ardhi binafsi na zoezi la majaribio la kuwaweka watu katika vijiji vya ujamaa liliwapokonya wananchi wote wa Tanzania wanaokaa hasa vijijini haki ya kumiliki ardhi na katika zoezi hilo la kuhamisha wengi walipoteza mali zao na nyumba zao na ardhi zao ambazo kuanzia mwaka 1974 wananchi hawa hawajawahi kupewa haki ya kumiliki ardhi.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuwamilikisha wananchi wa vijijini ardhi yao kwanza waliyoipoteza mwaka 1974 kabla haijawafikiria wawekezaji ambao si wengi wao na si wananchi wa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza si kweli kwamba Serikali imewazuia wananchi kumilikisha ardhi zao walizokuwa nazo baada ya vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 ilitangazwa Sera ya Ardhi ambayo inaruhusu wananchi kumilikishwa ardhi, nyumba na kadhalika kulingana na taratibu na sheria. Lakini pia ningemwomba Mheshimiwa Mbunge apitie Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 inayozungumzia masuala ya ardhi na kuwapa hati Watanzania wote katika kumiliki ardhi, ni mali ya vizazi vyetu. *(Makofi)*

Na. 11

**Mchanga wenye Dhahabu kutoka Bulyanhulu**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wawekezaji wa Sekta ya Madini wa Mgodi wa Bulyanhulu, huchukua mchanga ambao una dhahabu uliyounga na madini mengine aina mbili tofauti wakidai kwamba hapa Tanzania hakuna mashine ya kutenganisha madini hayo na dhahabu:-

(a) Je, Serikali inafaidikaje na hayo madini mengine baada ya kutenganishwa na dhahabu?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba madini mengine yanayopatikana baada ya kutenganishwa na dhahabu ni kiasi gani na yana thamani gani?

(c) Je, Serikali inafahamu ni kiasi gani cha dhahabu kinachopatikana kwenye mchanga huo unaosafirishwa nje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kwanza nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Kwa sababu za kijiolojia, mgodi wa Bulyanhulu unazalisha aina mbili za mazao. Vitofali vya dhahabu *(Gold Dores)* na koledhi ya shamba yaani *copper concentrate* ambayo Mheshimiwa Mbunge anaita mchanga wenye dhahabu.*Copper concentrate* inayozalishwa Bulyanhulu husafirishwa kwenda nchini Japan na China kwa ajili ya kutenganisha dhahabu na madini mengine ya shaba na fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kupata madini yaliyomo katika *copper concentrate* ni lazima yatenganishwe kwa kutumia teknolojia ambayo haipatikani hapa nchini. Teknolojia hiyo ni ya gharama kubwa na mtambo unaotumika unaotenganisha shaba na dhahabu unahitaji mtaji wa kiasi cha dola za Marekani kati ya milioni 400 hadi milioni 600 na mtambo huo ili uendeshwe kibiashara unahitaji kusafisha si chini ya tani za mizania laki moja nusu za shamba kwa mwaka ambazo zinapatikana kwa kusafisha tani za mizania laki nne za *copper concentrate.*

Kwa ulinganisho Mgodi wa Bulyanhulu huzalisha *copper concentrate* inayofikia tani za mizania 25,000 kwa mwaka ambazo huweza kutoa tani kati ya 5,000 hadi 9,000 tu za shaba. Kwa mantiki hiyo, siyo rahisi kujenga mtambo huo hapa nchini kwa vile hautakuwa na faida kibiashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kabla ya *copper concentrate* haijasafirishwa nje, vipimo vya maabara huchukuliwa kubaini kiwango cha madini yote yaliyomo na thamani yake. Wastani wa madini yaliyomo kwa kila tani moja ya *copper concentrate* ni gramu 6.8 za dhahabu, gramu 5.7 za fedha, na gramu 4.4 za shaba. Thamani ya madini hayo hutegemea bei ya soko siku ambapo *copper concentrate* inasafirishwa. Kulingana na tani zinazosafirishwa

na bei za siku hiyo, mrabaha wa asilimia tatu ya thamani ya madini hulipwa Serikalini kabla ya kutolewa kibali cha kusafirisha nje.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu (a) hapo juu, Serikali hupima na kufanya uchunguzi wa maabara kubaini viwango vya madini kwenye *copper concentrate* kabla ya kutoa kibali cha kusafirisha nje. Kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2005, kiasi cha shaba ya tani 3,469.5 yenye thamani ya dola milioni 4.6 na fedha ya tani 5.9 yenye thamani ya dola milioni 1.4 zilipatikana kutokana na *copper concentrate* iliyosafirishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005, mgodi wa Bulyanhulu ulisafirisha *copper concentrate* yenye madini ya dhahabu tani 5.6 yenye thamani ya dola milioni 79.1. Dhahabu hiyo ni nyingi ikilinganishwa na takriban tani 3 za dhahabu yenye thamani ya dola milioni 42.8 iliyopatikana katika zao la kwanza, yaani vitofali vya dhabu. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nina swali moja.

Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza jinsi Serikali inavyopata pesa kuhusiana na mgodi huo. Swali, je, ni lini wananchi wa eneo la Bulyanhulu watafaidika na matunda ya mgodi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuna faida nyingi ambazo tunazipata hapa nchini kutokana na migodi ambayo tunayo hapa nchini hasa katika eneo la Bulyanhulu. Taifa linapata *royalty* yaani mrabaha, Taifa linapata *income tax* na hivi sasa tunavyoongea Wizara ya Nishati na Madini imeingia katika maongezi na Mgodi wa Bulyanhulu pamoja na migodi mingine kuangalia namna ya kurekebisha mikataba hii ili kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yana migodi kama hii inafaidika zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 12

**Umeme Jimbo la Karagwe**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Karagwe katika kampeni zake alisikia kilio cha wananchi wa Karagwe kuhusu kutokuwa na umeme na aliahidi kuwapatia umeme hasa miji midogo ya Ihembe, Nyaishozi, Kyanyamisa, *Rugu World Vision,* Nyakaiga na Rwambaizi:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa sehemu hizo Jimboni Karagwe?

(b) Je, ni maeneo yapi yatakayopewa umeme jimboni Karagwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme *TANESCO* na Mtaalam Mshauri *SWECO* wanafanya upembuzi yakinifu wa kusambaza umeme maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Karagwe, yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Mtaalam Mshauri alizungukia maeneo hayo kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu mwezi Februari na Machi, 2006 na utayarishaji wa ripoti unaendelea.

Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA* ambalo ndilo limetoa fedha kiasi cha *Sek* milioni 2.5 za kufanyia upembuzi yakinifu. Imeonyesha nia ya kufadhili mradi huu ambao gharama yake itaainishwa na upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu uliofanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kayanga kuelekea Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi na Ihembe;

(ii) Kayanga kuelekea Lukaka, Kakiro, Nyabwengira, Lunyaga na Rwambaizi;

(iii) Kayanga kuelekea Rwebwera, Nkwenda, Kyerwa, Isingiro hadi Murongo; na

(iv) Rwebwera kuelekea Kamagambo, Nyakagoyegoye na Nyakaiga. *(Kicheko)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nashukuru kwa juhudi ambazo Serikali inafanya za kufanya upembuzi yakinifu katika jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu kwamba ni lini ripoti ya upembuzi yakinifu itakamilika na kuwasilishwa Serikalini? Hiyo ni (a).

Pili, baada ya ripoti hiyo ya upembuzi yakinifu kuwasilishwa Serikalini, je, ni hatua gani Serikali itachukua kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika haraka siyo unabaki kwenye karatasi? Ahsane Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ripoti ya upembuzi itapatikana mwishoni mwa mwezi Mei, 2006 na swali lake la pili, ningependa kumfahamisha kwamba pale tutakapopata ripoti ya upembuzi yakinifu Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha itawasilisha rasmi maombi kwa Serikali ya Sweden kwa ajili ya kupata fedha za kuanza mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa kuwa mipango ya Serikali kutokana na uwezo

inakwenda pole pole sana kupatia makao makuu ya Wilaya umeme. Je, Serikali inaweza ikaangalia uwezekano wa kupatia umeme mji wa Loliondo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro kutoka Jamhuri ya Kenya na hasa Wilaya ya Naroko? Je, uwezekano huo upo?

**SPIKA:** Naona kama ni swali jipya. Lakini kama Naibu Waziri ana majibu anaweza kujibu.Nadhani ningemshauri Mheshimiwa aliulize kama swali kamili lipate majibu kikamilifu. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 13

**Umoja wa Forodha**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY)** aliuliza:-

Kwa kuwa Ibara ya 75 ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inamaanisha kuwa Umoja wa Forodha *(Customs Union)* uundwe ndani ya miaka minne tokea kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki na kwa kuwa Jumuiya hiyo ilianzishwa tarehe 30 Novemba, 1999 na Umoja huo wa Forodha ukaanzishwa tarehe 2 Machi, 2004:-

(a) Je, ni sababu gani zilizochelewesha kusainiwa kwa makubaliano hayo ya umoja huo wa forodha?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutokamilika kwa orodha ya bidhaa kutokea Kenya ambayo inahusika na kuondolewa ushuru *(Duty Free Entry)* kwa kuingizwa Uganda na Tanzania ndio mwanzo wa kuzorotesha umoja huu wa Forodha?

(c) Je, ni bidhaa gani zilizoruhusiwa kuingizwa Zanzibar kwa njia ya msamaha wa aina hii ya kodi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Uwekaji saini makubaliano ya kuanzisha Umoja wa Forodha ulichelewa kutokana na sababu mbalimbali. Kwanza, nchi wanachama ilibidi zikubaliane misingi ya Umoja wa Forodha itakayotumika ili kuepuka makosa yaliyosababisha Jumuiya ya awali kuvunjika.

Pili, Tanzania, Kenya na Uganda zilikuwa na mifumo tofauti ya viwango vya kodi na hivyo kusababisha majadiliano kuhusu mfumo muafaka kuchukua muda mrefu.

(b) Orodha ya bidhaa kutokea Kenya ambazo zinahusika kuondolewa ushuru wa forodha pindi zinapoingizwa Uganda na Tanzania ilishakuwa tayari na inapatikana katika kitabu cha Forodha cha Afrika Mashariki. Bidhaa hizo ni zaidi ya 4,900. Bidhaa kutoka Kenya ambazo zinatozwa ushuru ni 840. Hata hivyo ushuru unaotozwa kwa bidhaa hizo utaendelea kupungua pole pole hadi kiwango cha sifuri ifikapo mwaka 2010. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kuvipa viwanda vya Tanzania vinavyozalisha bidhaa kama hizo za kutoka Kenya fursa ya kujiimarisha zaidi na hivyo kukabiliana na ushindani ifikapo mwaka 2010.

(c) Bidhaa zilizoruhusiwa kuingizwa Zanzibar kutoka Uganda na Kenya ni kama zilivyotajwa katika kitabu cha Forodha cha Afrika Mashariki kwa kuzingatia kanuni za uwasili wa bidhaa yaani *Rules of Origin* kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama. Bidhaa zinazohusika ni zaidi ya 4,900. Bidhaa hizo ni kama vile madawa, kemikali na malighafi. Msingi wa Kanuni za uwasili wa bidhaa lengo lake ni kuhakikisha kwamba bidhaa zinazopatiwa unafuu wa ushuru wa forodha zinapoingia katika soko la Tanzania ziwe kweli ni za Uganda au Kenya na siyo vinginevyo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa ukitaja mmwaka 2010 utaona iko mbali lakini uhalisi wa mambo inaonyesha iko karibu sana hasa katika suala la kuimarisha viwanda. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa muda huo ni mdogo na inapaswa suala hili lijadiliwe ili kuongeza muda wakupe fursa ya kuimarisha viwanda vya Tanzania? Hilo la kwanza.

Lakini la pili, katika mchakato huu kuna faida na hasara. Kwa kuwa sisi hivi sasa viwanda vyetu havizalishi sana, je, tunapoteza fedha kiasi gani kwa kupokea bidhaa nyingi kutoka Kenya katika wakati huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza jambo linalotakiwa hapa ni kuhakikisha tunaimarisha viwanda vyetu. Tunaendelea kutekeleza sera zetu za kuvutia wawekezaji wengi zaidi na kuweka mazingira kama jitihada mbalimbali zinavyofanyika.

Lakini vile vile hatuwezi kulinda uzalishaji mbovu milele. Kwa hiyo, natoa wito kwa wazalishaji wote na kwa Watanzania wote kuchukua jitihada zinazowezekana ili kuhakikisha ifikapo mwaka 2010 viwanda vyetu viweze kushindana. Kama tukishindwa tutaangalia tufanye nini kwa sababu taratibu zinaturuhusu lakini lazima tufanye jitihada za makusudi za kuhakikisha tunaimarisha viwanda vyetu.

Pili, kwa kuruhusu bidhaa kutoka Kenya kuingia Tanzania hatupotezi fedha zozote kimsingi. Kwa sababu na sisi vile vile tunaruhusiwa bidhaa zetu kuingia Kenya bila ushuru wowote. Kinachotakiwa ni kutumia fursa hiyo ili kuweza kuzalisha zaidi. Lakini la mwisho natoa wito kwa Watanzania tusiogope sana Kenya huku yako Mataifa mengine makubwa kama China, Malaysia na mengineyo. Tunaweza tukafunga mipaka

ya Kenya je, tutafunga ya Kichina? Je, tutafunga ya Malaysia? Tuko katika utandawazi lazima tujizatiti kukabiliana na hali hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD R ASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wakati huu sisi Kenya tayari wameshatuzidi na kwa kuwa tumeweka kipindi cha mpaka mwaka 2010 na kwa kuwa wao vile vile wanaendelea. Hatuoni kwamba siyo *realistic* kuweka huu muda wakati wao hawa-*mark time* kutusubiri sisi?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kihistoria kwamba Kenya wana viwanda vingi na imara kuliko Tanzania na ndiyo maana katika kutambua hilo mkataba wa makubaliano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unazingatia sana tofauti iliyopo kati ya nchi zetu tatu. Sasa kuhusu miaka mitano ya mpito tunazo hizi bidhaa kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, tunazo hizi bidhaa 840 za kutoka Kenya zinapoingia Tanzania tunatoza ushuru na kwa upande wa Uganda zipo bidhaa 430 ambazo kutoka Kenya zinapoingia Uganda zinatozwa ushuru. Lengo ni hilo hilo kwamba tuimarishe viwanda hivi katika kipindi hiki cha mpito na kama tulivyojibu katika swali la msingi, viwanda hivi vya Tanzania sasa hivi vinafanya vizuri na vitaendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona bidhaa ambazo sasa hivi Tanzania inauza Kenya tangu itifaki ya Ushuru wa Forodha ianze kutumika, ni bidhaa nyingi na ni bora. Mimi rai yangu kwa Watanzania wafanyabiashara ni kwamba tuendelee kuzalisha bidhaa zilizo bora na zitangaze sana ili wananchi wazifahamu na pia tuwe na uzalendo wa kupenda bidhaa zetu. *(Makofi)*

Na. 14

**Tatizo la Wakimbizi na Ujambazi**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma kwa muda mrefu umekuwa unapokea wakimbizi kutoka nchi jirani za Burundi na *Congo (DRC)* na kuwahifadhi kwenye makambi na kwa kuwa baadhi ya wakimbizi hao wanashiriki katika vitendo vya ujambazi kwa kuvamia wananchi na kupora mali zao kwa kutumia silaha wanazokuja nazo na kwa kuwa wananchi wengi wamekwishapoteza maisha yao na kupata vilema vya kudumu kutokana na ujambazi huo:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kurejesha imani na amani kwa wananchi wa Wilaya ya Kibondo kwa kutokomeza ujambazi wa silaha?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mipaka yetu na kuhakikisha kuwa silaha haramu haziingii nchini?

(c) Je, wakimbizi 3,00 walioingia Kibondo Februari, 2006 wakidai kukimbia njaa na usumbufu wa majeshi ya waasi nchini kwao wasingeweza kushughulikiwa nchini kwao hasa baada ya muafaka wa ndani ya nchi yao kupatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda maarufu Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuwepo kwa wakimbizi katika Mikoa ya Kagera na Kigoma kumesababisha kuongezeka kwa matukio ya uhalifu hususan ujambazi wa kutumia silaha na utekaji wa magari *highway robbery.*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inatokana na baadhi ya wakimbizi hususan wapiganaji *ex-combatants* na vikundi vya waasi kutoka nchi za Burundi na *Congo (DRC)* kukimbilia nchini na silaha zao na kutosalimisha silaha hizo kwa mamlaka husika katika maeneo ya mapokezi na kusababisha silaha kutumika katika matukio ya uhalifu.

Kwa kuzingatia matukio ya uhalifu yanayojitokeza katika mikoa inayohifadhi wakimbizi ikiwemo Wilaya ya Kibondo, Serikali inafanya jitihada zifuatazo katika kudhibiti hali hiyo:-

(i) Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR)* imeweka mpango maalum wa ulinzi ujulikanao kama *Security Pakage* chini ya mpango huo, Serikali hupeleka askari Polisi wa ziada katika mikoa inayohifadhi wakimbizi kwa ajili ya kulinda makambi ya wakimbizi na kufanya doria katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka makambi hayo.

(ii) Serikali hufanya misako ya majambazi *(operations)* mara kwa mara katika maeneo hayo. Operesheni hizi hushirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini.

(iii) Serikali inatekeleza mpango wa kuwarejesha wakimbizi kwenye nchi zao za asili ikiwa ndiyo suluhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi na madhara yanayotokana na kuwepo kwao.

(iv) Serikali inawachukulia hatua za kisheria wakimbizi wanaokamatwa na silaha na kujihusisha na vitendo vya ujambazi na uporaji. Hatua hiyo ni pamoja na watuhumiwa kushitakiwa na baadaye kutumikia adhabu zinazostahili.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi wa mipaka yetu, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mipaka yetu yote inalindwa kwa ukamilifu na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania. Hadi sasa mipaka yetu yote ya kule ni shwari.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kati ya Januari hadi Machi, 2006 tulipokea wakimbizi wapya 11,379 toka Burundi lakini tumekataa kuwapa hifadhi ya ukimbizi kwa kuwa baada ya kuwahoji kwa kweli tumeona walikimbia njaa. Aidha, Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia wakimbizi na *World Food Programme* pamoja na *UNICEF* wameandaa mpango wa dharura wa kuwapelekea chakula huko huko kwao baada ya Serikali ya Tanzania kuwaomba wafanye hivyo. Utekelezaji wa mpango huu ambao utaanza mwezi ujao utawafanya wakimbizi hao wa njaa warudi kwao katika maeneo walikotoka ili wakapate chakula huko huko.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Hadi jana tarehe 27 Machi, 2006 wakimbizi ambao wako kwenye *refugee way stations* wamefika 12,002 na wakimbizi ambao wako kwenye makambi manne niliyo nayo kwenye jimbo langu ni 63,897. Sasa kwa utaratibu wa wakimbizi hao kuingia na silaha ambayo inasababisha vitendo vya ujambazi vishamiri katika jimbo hilo.Nilikuwa nadhani muda muafaka sasa kabla hawajarudi huko kwao. Hao wakimbizi wapekuliwe kwa sababu wanapoingia ndiyo wanaingia na silaha hizi zinazofanya ujambazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, labda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu. Lakini kama anasema kuna misako inayofanyika kwa madhumuni ya kuwakamata majambazi halafu na misako hiyo hiyo inakamata silaha ambazo zinaingizwa *I mean* zinaingizwa na wakimbizi hao wanaokuja kufanya vitendo vya ujambazi.

Nilikuwa nadhani pia kwamba ni muda muafaka Mheshimiwa Waziri angeweza kunieleza na kumweleza mwananchi wa Jimbo la Muhambwe ama Wilaya ya Kibondo ili tuweze kujua ni majambazi wangapi wamekamatwa katika msako huo na pili ni silaha ngapi zimekamatwa katika msako huo ili mwananchi wa Muhambwe aweze kuishi kwa imani na amani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri ni kweli tuna wakimbizi hadi sasa waliopo kwenye makambi yetu 69,000 na nakiri pia kwamba hadi tarehe 15 Machi,2006 tulikuwa na wakimbizi njaa kwenye vituo vya *way stations* waliokuwa 11,379. Lakini hata nilipokuwa kule na Mheshimiwa Spika, ningependa kukuhakikishia nilikwenda Kibondo kuangalia hali hii. Watu 200 walikuwa wanaingia kila siku na kwa hiyo takwimu alizozitoa Mheshimiwa Mbunge ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli wanapoingia pia wanapekuliwa. Lakini pili, ametaka kujua kama Serikali inafanya kazi yake na ningependa kutoa takwimu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja wakimbizi majambazi 138 walikamatwa. Katika hao 70 walikuwa wanahusika na mauaji. 24 walikamatwa na silaha pamoja na risasi na 34 walihusika na makosa ya wizi wa kutumia silaha na 10 walihusika na makosa ya kubaka. Jumla ni 138. Lakini wote hao walikamatwa na kwa upande wa silaha zilizokamatwa katika kipindi cha miezi sita

iliyopita ni silaha 148, zikiwemo bastola, magobore pamoja na bomu la mkono. Yote hayo yamekamatwa.

Ningependa nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Siasa ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kibondo kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ningependa nichukue nafasi hii kuwashukuru vijana wetu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama hasa Polisi ambao pamoja na matatizo magumu wanayoyapata mpakani, wanafanya kazi inayostahili heshima na lazima tuwapongeze watu hawa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 15

**Utekelezaji wa Sheria ya *Parole***

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na mambo mengine Sheria ya *Parole inalenga* kupunguza msongamano wa wafungwa katika Magereza:-

Je, tangu sheria hiyo ianze, ni wafungwa wangapi wamepata msamaha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bodi ya *Parole* ilitungwa mwaka 1994 na Bodi ya kwanza ya Taifa ya *Parole* ilikaa kikao chake cha kwanza mwaka 1999 ambapo wafungwa watatu tu ndio waliachiliwa baada ya kutimiza masharti yaliyomo katika sheria hiyo.

Katika kikao cha kwanza cha Bodi kilichofanyika, ilibainika kuwa Sheria hiyo ilikuwa haikidhi matarajio ya uanzishwaji wake. Hivyo Bodi ilitoa mapendekezo Serikalini kwamba Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ya kulegeza masharti na kupanua wigo na kuruhusu wafungwa wengi zaidi kufaidika nayo.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliifanyia marekebisho Sheria hiyo mwaka 2002 ambapo wigo ulipanuliwa kuwawezesha wafungwa wengi zaidi kufaidika. Tangu Sheria hiyo ilipofanyiwa marekebisho hadi kufikia Desemba, 2005 wafungwa 1,727 walifaidika na kufanya jumla ya wafungwa walioachiwa kuwa 1,730 tangu itungwe Sheria hii ya *Parole.*

Hata hivyo bado upo umuhimu kwa Sheria hii kuangaliwa tena upya ili kupanua zaidi wigo kuwawezesha wafungwa wengi zaidi kuachiliwa kwa utaratibu huo wa *Parole.*

Hivi sasa wafungwa wengi wa vifungo virefu waliopo magerezani wamejirekebisha kitabia, lakini hawawezi kunufaika na Sheria hii kwa jinsi ilivyo sasa.

**SPIKA:** Nawasihi wanaouliza maswali ya msingi inapokuwa nyongeza wachangamke. Vinginevyo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Spika jicho lake linaangalia yule ambaye amejitokeza haraka. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa maelekezo yako. Lakini pia uangalie na hali halisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kifungo kinalenga kumwadhibu mtu, lakini pia ni lengo lingine la kumfanya mtu kujirekebisha. Nilikuwa naomba kujua ni nini kinafanyika, mchakato unaofanyika ili kuwasaidia au kuwarekebisha hawa wafungwa ili waweze hata ku-*qualify* kunufaika na msamaha huu wa *Parole?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika Magereza yote ya nchi kuna *Parole Boards* zinazoangalia tabia za wafungwa wetu. Hilo siyo tatizo. Tatizo ni kwamba Sheria hii inataka baada ya kuwaona watu waliojirekebisha kufaa kuachiwa, inabidi moja, wananchi wa sehemu ile alikotoka mhalifu wakubali kwamba huyu baada ya kutumikia theluthi moja ya umri wake wa magereza sasa anaweza kurudi nyumbani. Sasa hilo linakuwa gumu sana kwa wananchi kulikubali.

Lakini pili, *victims* yaani wale walioathiriwa na yule inabidi pia nao wakubali kabla hajaondolewa gerezani kwamba na wao wanakubali arudi akakaye nyumbani.

Sasa kwa uzoefu ni kwamba wananchi hawataki kusema hivyo na kwa sababu hawataki kufanya hivyo, hawa vijana ambao wame-*qualify* kuondoka kwa mujibu wa *Parole* wanashindwa kutoka magerezani, kwa sababu wananchi pamoja na wale walioathirika na tukio hilo hawapo tayari. Ndiyo maana tulisema ni vizuri Sheria hii kuiangalia upya ili kupanua wigo na kuondoa vitu hivi ambavyo vinakwamisha jitihada za magereza kupunguza msongamano kwenye magereza yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia wa maswali umekwisha. Baada ya hapa kama tulivyokubaliana jana tutakuwa na ile Semina muhimu sana kuhusu ile Miswada ya kifedha na hususan ule Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Benki Kuu.

Mwenyekiti wa Semina hiyo atakuwa ni Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tuwemo humu ndani hasa kwa ule Muswada wa Benki Kuu. Ni mrefu, mzito na una mabadiliko makubwa katika Sheria nzima na hasa mustakabali wa namna ya kuendesha uchumi kwa siku za usoni kwa nchi yetu.

Kwa hiyo, ni Muswada muhimu na kama tulivyokubaliana basi hiyo Semina itaanza mara baada ya kipindi cha maswali, nawasihi msiende mbali. Sekretarieti watagonga kengele, tutarejea hivi punde. Nadhani haitachukua zaidi ya dakika tano si zaidi ya kumi tutakuwa tayari ndani ya Bunge.

Baada ya kusema hayo sasa naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi, saa tatu hapa hapa katika Ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

*(Saa 04.30 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, tarehe 29 Machi, 2006 saa tatu asubuhi)*